

Jumbe taka

Kwa kila kisa, tambua ikiwa ujumbe huo ni taka na ikiwa unafaa kusambaza taarifa kwa mtu huyo. Tafadhali andika jibu la kila swali kwenye sehemu zilizoachwa wazi.



KISA CHA 1: Unapokea ujumbe kuto kampuni fulani unaokujulisha kwamba umeshinda kitita cha pesa katika shindano. Hata hivyo, ili uweze kupokea pesa hizo, wanahitaji namba ya akaunti ya benki ya mzazi wako.

Kuna uwezekano mkubwa kwamba ujumbe huo ni taka. Kutoa taarifa za akaunti yako ya benki ni hatari wakati wote na inatakiwa ifanyike kwa umakini. Kamwe usimtumie mtu taarifa zako isipokuwa kama wewe ndiye uliyewasiliana naye kwanza, na pia katika hali hiyo, kuwa mwangalifu sana. Kwa mfano, huenda sio vizuri kutuma taarifa zako kupitia ujumbe wa simu kwa kuwa hujasimbwa. Hii ndiyo sababu hospitali, wanasheria na mabanki mengi huwa na tovuti maalum zinazotumiwa kuwasiliana nawe.



KISA CHA 2: Rafiki anakutumia ujumbe, akikujulisha kwamba anajaribu kutafuta picha uliyomwonesha hapo awali lakini hana ruhusa ya kuitazama. Huwezi kuipata kompyuta yako sasa hivi ili kumtumia picha hiyo. Anakujibu kwa kusema, "Ninaweza kuingia kwenye akaunti yako kwa muda mfupi ili nipakue picha hiyo — nywila yako ni ipi?"

Ingawa huu sio ujumbe taka, hutakiwi kuwapa watu wengine nywila zako. Mara tu wanapozipata nywila zako, wanaweza kukuzuia usiingie katika akaunti hiyo au usiweze kuingia katika akaunti zingine za mtandaoni zinazotumia nywila inayofanana na ya akaunti hiyo. Aidha, ikiwa mhusika wa tatu, mdukuzi, au mtazamaji ataona ujumbe wako, watu wengine wanaweza kuingia katika akaunti yako bila wewe kujua.



KISA CHA 3: Unapokea barua pepe iliyotumwa kwako kutoka shuleni kwako, inayodai kwamba akaunti nyingi za wanafunzi zimedukuliwa. Inadai, "Hivi karibuni tumetambua kwamba akaunti nyingi za wanafunzi zimedukuliwa. Tunaomba msamaha na tunajitahidi kulishughulikia tatizo hili. Ili kuirekebisha tena akaunti yako, tafadhali jibu barua pepe hii kwa jina la mtumiaji na nywila yako."

Ni kawaida kwamba watumiaji hawaombwi kutoa taarifa hizi. Hata ikiwa aliyetuma barua pepe anaonekana kuwa wa kuaminika, unatakiwa kuchukulia kwamba barua pepe yoyote inayokuomba nywila yako ni taka.



KISA CHA 4: Unapokea barua pepe kutoka katika benki yako ambako una akaunti halisi. Barua pepe hiyo inasema kwamba akaunti yako imedukuliwa na unahitaji kuingia kwenye akaunti ili kubadilisha nywila yako haraka iwezekanavyo na ubadilishe nywila za akaunti zozote zinazotumia nywila sawa na akaunti hiyo.

Hatua unayofaa kuchukua ni kufungua dirisha jipya kwenye kivinjari na kuingia kwenye tovuti kama unavyoingia kwa kawaida. Kutolewa kwa habari ya aina hii (kwamba akaunti zimedukuliwa) kwa kawaida huwekwa kwenye tovuti ya wateja ya kampuni au benki. Maelekezo yaliyo kwenye tovuti hiyo yanatakiwa kufuatwa kwa njia salama. Kama ilivyo kwenye Kisa cha 3, hakuna mtu yeyote wa kuaminika atakayekuomba maelezo ya akaunti yako kupitia barua pepe.

Chanzo: Maudhui haya yanahifadhiwa na Meta na hivi sasa yanajumuisha mafunzo yaliyotolewa kwa shirika la Youth and Media katika Kituo cha Berkman Klein cha Intaneti na Jamii katika Chuo Kikuu cha Harvard chini ya leseni ya Kimataifa ya Creative Commons Attribution-ShareAlike 4.0. Unaweza kuyatumia maudhui hayo, ikiwa ni pamoja na kuyanakili na kuandaa kazi zinazotokana na maudhui hayo, kwa madhumuni ya kibiashara au la, ilimradi utataja mradi wa Youth and Media kama chanzo cha asili na kufuata masharti mengine ya leseni hiyo, kushirikisha kazi zingine zozote za ziada chini ya masharti hayo.